**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti:http://www.utumishi.go.tz

Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
**40404 DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**WANAWAKE WAASWA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA MAARIFA**

Wanawake katika sekta ya umma nchini wametakiwa kufanya kazi kwa juhudi, bidii, maarifa na weledi ili kutoa mchango katika maendeleo ya taifa badala ya kutegemea upendeleo (***favoritism***) mahala pa kazi.

Wito huo umetolewa leo na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Dorothy Mwaluko wakati wa Maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI kwa lengo kuhamasisha uwajibikaji kwa wanawake kuelekea uchumi wa viwanda.

Bi. Mwaluko amewaasa watumishi wa umma wanawake kuzitendea haki ajira zao badala ya kupoteza muda mwingi kupiga soga kazini, kulalamika na kujiona kuwa ni kundi linaloonewa mahala pa kazi.

Amesema kuwa nafasi ya mwanamke katika ujenzi wa taifa ni kubwa, hivyo ametoa angalizo kwa wanawake nchini kutumia maadhimisho haya kutafakari kwa kina namna bora ya kutoa mchango katika nyanja ya maendeleo.

Aidha, Bi. Mwaluko amewatahadharisha wanawake kutotumika kutoa siri za Serikali kwa kurubuniwa na zawadi, na amewataka kuwa wasiri na waaminifu ili waweze kupata fursa za uongozi na kushiriki kutoa maamuzi yenye tija kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama msimamizi wa sera na miongozo inayohusu rasilimaliwatu imeungana na wadau wengine nchini kuhamasisha nafasi ya mtumishi mwanamke katika kuchangia uchumi wa viwanda.

Sanjali na hilo, watumishi wanawake wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wameadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kuongeza muda wa ziada wa kutoa huduma tofauti na saa za kawaida za kazi kuanzia tarehe 06 Machi hadi leo tarehe 8 Machi, 2018.

Pia watumishi hao wameendesha mjadala kuhusu nafasi ya mwanamke kuelekea uchumi wa viwanda na kutoka na maazimio yatakayoboresha utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na kupata fursa ya kupima Saratani ya matiti, Kizazi, Kisukari na Shinikizo la Damu ili kutambua hali ya afya zao na kuchukua hatua stahiki kwa lengo la kuboresha utoaji huduma katika Utumishi wa Umma.

Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu ni "***KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA: TUIMARISHE USAWA WA KIJINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE VIJIJINI***".

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**OFISI YA RAIS (UTUMISHI)**
TAREHE 08 MACHI, 2018